

Mnyauko bakteria kwenye nyanya

Tambua tatizo

Bakteria mnyauko ni ugonjwa unaoweza kujitokeza katika hatua zote za ukuaji wa mmea. Kwanza unajionyesha kwa kunyauka kwa majani ya machanga, baadaya siku mbili au tatu mmea wote hunyauka haraka bila majani kubadilika na kuwa ya njano. Shina la mmea ulioathirika hubadilika na kuwa na rangi ya kahawia. Shina la mmea ulioathirika likikatwa na kulowekwa kwenye glasi ya maji ndani ya dakika moja, linatoa utomvi mfano wa maziwa kuonyesha kwamba bakteria wanatoka.

Habari tangulizi

Mnyauko bakteria ni ugonjwa unaopatikana kwenye udongo na unaathiri mimea kupitia kwenye mizizi au shina. Vilevile hambukizwa kupitia sehemu ya mmea yenye jeraha lililosababishwa na vifaa vya kilimo au minyoo fundo. Pia huishi kwenye mazao ya familia moja na nyanya kama blinganya. Husambaa vilevile kwa rija ya maji ya umwagiliagi na mbegu. Ni rahisi kuzuia / kakinga kuliko kutibu.

Usimamizi

- Tumia aina ya mimea inayostahimili ugonjwa (Fortune Maker, Kentom, Taiwan F1).
- Usioteshe nyanya maeneo ya bondeni ambayo daima ni maji maji na yenye historia ya mnyauko bakteria
- Fanya mzunguko wa nyanya na mazao mengine yasiyo ya jamii ya nyanya kama vile nafaka, kunde, miwa, kabichi na siyo pilipili wala viazi mviringo
- Epuka kuhamisha vifaa/vyombo/maji kutoka eneo lenye ugonjwa kwenda eneo lisilo na ugonjwa.
- Simika miti wiki mbili baada ya kupandikiza miche na punguza majani ili kuipa mimea hewa. (angamiza vijidudu kwenye visu vilivyotumika kwa kutumia blichu kabla ya kutumia kwenye mmea mwingine).
- Epuka umwagiliagi wa kutumia mifereji kwa kuwa hueneza ugonjwa huu ulio kwenye udongo haraka zaidi. (kama unatumia mfereji, anza kumwagilia eneo jipya kuelekea lile la zamani).

Endapo utagundua mmea mmoja umeathirika katika shamba lako chukua hatua ya kututhibiti ugonjwa.

- Ng'oa mmea, mizizi na udongo wa eneo hilo na kuchoma vyote, usivibebe vikiwa wazi kwenye shamba kwani vitaeneza ugonjwa, usioteshe tena nyanya kwenye shimo hilo.
- Unaweza kupunguza mashambulizi kwa kunyunyiza sumu aina ya copper oxychloride au copper hydroxide, zote ni sumu hatari (daraja la II WHO). Vaa vifaa vya kujikinga nyunyiza dawa siku 14 kabla ya kuvuna.

Mimea yote inaweza kunyauka haraka kutokana na ugonjwa wa mnyauko. (Picha na A. Massawe)




Rangi ya kahawia ya shina lenye ugonjwa huu. (Picha na UGA)



Wakati wa kutumia kemikali, vaa mavazi ya kinga wakati wote na ufuate maelekezo kwenye lebo ya bidhaa, kama vile kipimo, majira ya kuweka, muda kabla ya kuvuna

Jina la kisayansi > *Ralstonia solanacearum*

Mapendekezo katika vidokezo hivi yanatumika katika: Tanzania



WAANDISHI: Adeltruda Massawe, Mansuet Tilya, Martin Kimani, Richard Musebe, Livin K Mahoo, Irene Kessy
Horti Tengeru, Tanzania

Mwisho na Plantwise.